PANDA MITI KIBIASHARA
PRIVATE FORESTRY PROGRAMME

# UZALISHAJI WA VITALU VYA MICHE NCHINI TANZANIA

## Taarifa za jumla

- Uzalishaji wa miche ni hatua muhimu katika mnyororo thamani wa misitu, kama ilivyo kwa mkate huwezi kutengeneza mkate kwa unga ulioharibika, Uahitaji mbegu bora za miti ili kuotesha misitu bora.
- Miche iliyo bora hutoka katika vitalu vya kitaalamu vya mbegu ambavyo vinazalisha mbegu zilizoboreshwa. Mbegu hizi zinatoka katika vyanzo vya miti iliyoboreshwa vinavyotambulika zinazoota kwa uwezo wote. Hivyo inapendekezwa matumizi ya mbegu zilizoboreshwa kwakuwa zinakuhakikishia miti yenye ubora, kiwango kikubwa cha ukuaji na uhalisia wa mbegu.
- Zipo aina mbili za vitalu nchini Tanzania: Kitalu cha viriba vya plastiki na kitalu cha trei/chano ya miche. Faida kubwa ya kitalu cha viriba vya plastiki ni ustadi wa miche, inayofanywa kuwa na uvumilivu zaidi wakati wa kubebwa na kusafirishwa. Ingawa, njia hii huifanya iwe mikubwa na mizito kusafirishwa, kwa mfano wakati wa usafirishaji trei za miche zinaweza kubebwa mara tatu zaidi ikilinganishwa na viriba vya miche.

## Mambo ya kuzingatia kabla ya kuanzisha kitalu cha miti

- Tathmini ya upatikanaji wa soko la uhakika inahitajika ili kubaini uwepo wa wanunuaji wa kutosha wa miche yako. Lengo hili laweza kufikiwa kwa kufanya utafiti wa soko kabla ya msimu wa kupanda ili kujua kiwango cha uhitaji. Unaweza kujitengenezea orodha ya awali ya oda za wateja, na ili uwe na uhakika unaweza ukazungumza nao kwa ajili ya malipo ya awali na tarehe za kufikisha miche
- Unapoanzisha kitalu, yakupasa utathmini ukubwa wa ardhi unyohitaji kwa ajili ya kitalu chako. Unapokadiria mauzo yako kabla ya msimu wakati wa tathmini ya soko la miche, unaweza kupiga hesabu ya kuwa kila heka ya ardhi anayotaka kupanda mteja wako inahitaji miche 600. Hii inamaana kwamba, kama umeanzisha kitalu cha miche 400,000 unaweza kuuza miche ya kuweza kutosha heka 700 za msitu.
- Ukubwa wa ardhi inayohitajika hutegemea na ukubwa wa kitalu: kwa wastani 1/2 heka huhitajika kwa miche 400,0000..
- Pia unatakiwa kuchagua aina/jamii ya miti inayofaa. Unapochagua aina/jamii ya miti inayofaa, zingatia uhitaji na uendelezaji wa jamii hiyo kwa ajili ya maeneo ya kupanda ambayo unahudumia, hali yake ya hewa, mwinuko na aina ya udongo.
- Unapochagua eneo kwa ajii ya kitalu chako, hakikisha eneo hilo liko sawa na lisilotuwamisha maji na lina ubora mzuri, lenye chanzo endelevu cha maji.Tazama picha namba 4 kwa utengenezaji kitalu katika mteremko.
- Utahitajika kuchagua kati ya kitalu cha viriba vya plastiki ama kitalu cha trey. Tambua kuwa katika kitalu cha viriba vya plastiki, miche inaweza kuwekwa chini, lakini kwa kitalu cha trei miche inatakiwa kuwekwa juu ya kichanja ili kuwezesha upunguzaji wa mizizi. Tazama picha namba 1 na 2 hapo chini.

## Uanzishwaji wa kitalu

- Aina za miundo na malighafi zifuatazo zinahitajika katika kitalu cha miti kilichoanzishwa vyema:
  - Vichanja vya kuoteshea, kama vitahitajika, viwe na njia kati ya vichanja kwa ajili usimamizi wa miche.
  - Vichanja vya miche (mistari ya miche katika viriba ama katika trei).
  - Kivuli kwa ajili ya vifaa, dawa na utawala.
  - Chanzo cha maji: kwa tenki au kwa kisima.
  - Zana za kuoteshea (umbo lenye matundu): udongo, makapi ya ganda la nje la nazi, Makapi ya mpunga yaliyotiwa mkaa, gome la mpaina. Vyombo vya kuoteshea vipimwe ili kuhakikisha ni visafi, visivyo na magonjwa ama visivyo na mbegu nyingine.
  - Kitambaa cha kivuli (kinachozuia asilimia 15 ya jua na kuzuia mvua wakati wa mvua ya mawe au mvua kubwa).
  - Wafanyakazi waliopata mafunzo. 1/2 heka ya kitalu inahitaji wastani wa timu ya watu 10.
- Miche ya kuanzishia kitalu inaweza kupandwa moja kwa moja kwenye tybu au trei (inashauriwa), ama katika kitalu kidogo cha kuoteshea mbegu na kasha kuihamishia katika tyubu au trei baada ya kuota.
- Unasisitizwa kutumia mbegu zilizoboreshwa, kwakuwa mbegu hizi zitakuhakikishia bidhaa bora kwa wateja wako. Unaweza kuona utofauti kati ya mbegu za kienyeji na zile zilizoboreshwa katika picha 2 hapo chini. Miche ya kijani kibichi ni ya kienyeji inayotoka na mbegu zinazokusanywa katika mipaina ya kijiji wakati miche ya kijani mpauko ni ile inayotolewa na mradi wa Panda Miti Kibiashara inayotokana na mbegu zilizoboreshwa.
- Umwagiliaji waweza kufanywa kwa kutumia mfumo wa kunyunyiza maji (sprinkler) au inaweza kufanyawa kwa kutumia keni za kumwagilia.
- Uwekaji wa mbolea unaweza kuanza baada ya mwezi mmoja wa kupandwa mbegu kwa kiwango kidogo cha mbolea ambacho huongezwa taratibu kadri miche inavozidi kukua.



Picha 1. kitalu cha trei



Picha 2. Kitalu cha viriba



Picha 3. Kivuli




Picha 4. ujenzi wa mteremkoni na utunzaji

## Usimamizi wa kitalu

- Marekebisho ya mara kwa mara, ikiwema hali nzuri ya usafi na upaliliaji ni mambo muhimu katika mafanikio ya uoteshaji miche.
- Hatari ipo katika kuzidisha au kupunguza umwagiliaji wa miche kupita kiasi, magonjwa ya mimea na kuzidisha kiwango cha mbolea.
- Uwepo wa fangasi, kuvu ama magonjwa yanayosababishwa na wadudu hatua kama kutupa na kuharibu miche iliyoathirika na matumizi ya madawa ya kuvu na wadudu, lazima zichukulie. Utakapotambua ugonjwa, haribu mche ulioathirika mbali na mazingira ya kitalu, usiuharibu karibu na mazingira ya kitalu.
- Kwa kesi ya ugonjwa pia tupa vifaa vya kukuzia mche ulioathirika na ugonjwa. Usivitumie tena (kwasababu vina vimelea vya ugonjwa na vinaweza kusababisha matatizo mche utakaooteshwa upya)
- Uwekaji alama katika miche na utunzaji wa kumbukumbu ni muhimu; weka alama katika kila kundi la miche ili kuweza kuwapa wateja kundi sahihi la miche.
- Hata kama unafuata vizuri taratibu zote za utunzaji wa miche, matatizo ya magonjwa huweza kutokea. Tegemea (na upigie hesabu katika gharama zako za uzalishaji) hasara ya asilimia 5-10 kabla ya kuanza uzalishaji. Hii inamaana kuwa ongeza bei ya miche ili kufindia hasara.
- Miche inayotoka kwenye kitalu ni lazima imwagiwe maji vizuri.
- Itunze miche kwa uangalifu mkubwa ili udongo ulioshikilia mizizi usiachie.

## Kalenda za shughuli za misitu




**Huduma zinaohusiana na shughuli za vitalu vya miche katika kituo.**

- Huduma ya maelezo
- Uzalishaji wa miche kwa ajili mashamba ya mbegu nchini Tanzania.
- Kuwapa mafunzo wajasiria mali wa vitalu vya miti katika uanzishaji na utunzaji.

**Msaada unaotolea na mradi kwa mashamba ya mbegu za miti.**

Hivi sasa shamba la mbegu bora la taifa limepungukiwa uwezo na hivi kumudu kuhudumia mahitaji ya serikali tu. Kutoa majibu ya mahitaji ya wamiliki binafsi wa vitalu vya miti na wakulima wa binafsi wa miti, mradi wa Panda Miti Kibiashara unaendeleza hekta 150 za shamba la mbegu ndani ya nyanda za juu kusini kwa kushirikiana na Muungano wa Vikundi vya Wakulima wa Miti Tanzania. Inategemewa kuwa mashamba haya ya mbegu yatamudu kujibu maswali ya uhitaji wa mbegu kwa nchi nzima ndani ya muongo mmoja.

**Mawasiliano na namna ya kufika kituoni**

Kituo cha Mafunzo ya Viwanda vya Mazeo ya Misitu (KMVMM)

Kinyanambo

Mafinga

Mr. Edigary, Mwaifweya Meneja wa Kituo.

Barua pepe: edigary.mwaifweya@privateforestry.or.tz

Tel: +255 744 874 521

Maelezo kwa watumiaji magari: Njia panda ya kituo cha Mafuta cha CF, barabara iendayo Madibira, endesha umbaki wa kilomita moja. Utaona kibao cha kituo upande wa kushoto mwa barabara, mkabala na kiwanda cha mkaa.

**Kuhusu Programu ya Panda Miti Kibiashara PFP)**

Pandamiti Kibiashara husaidia umiliki binafsi wa mashamba ya miti hasa katika uanzishwaji na utunzaji wa mashamba ya miti kwa wakulima wadogo, kadhalika viwanda vya mazao ya misitu pamoja na ukuaji wa soko la mazao ya mbao yaliyokomaa ambayo yatanufaisha wadau wote. Programu inatekeleza katika Mikoa minne: Iringa, Njombe, Morogoro na Ruvuma.

Mradi unafadhiliwa na Wizara ya Mambo ya Nje ya Finaland na Wizara ya Maliasili na Utalii ya Tanzania

United Republic of Tanzania
MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM
Forestry and Beekeeping Division

FORMIN.FINLAND.FI
MINISTRY FOR FOREIGN AFFAIRS OF FINLAND

© Private Forestry Programme 2018